**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

**MHESHIMIWA MASOUD ALI MOHAMMED**

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

**IMEWASILISHWA MBELE YA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

**MEI,2025**

## A.UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai, uzima na kutukutanisha hapa tukiwa na afya njema tukaweza kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kuwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

2. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kwa madhumuni ya kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji ya miezi tisa (Julai-Machi) 2024/2025 na hatimaye kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

3. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutumia nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zao wanazozichukua kudumisha amani, utulivu, mshikamano na kuleta maendeleo ya Taifa letu.

4. **Mheshimiwa Spika,** nichukue nafasi hii kuendelea kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuteuliwa kwao kuwa wagombea pekee wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa nafasi za urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na urais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

5. **Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii adhimu kumpongeza na kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Hussein

Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambae pia ni Kamanda Mkuu wa Idara Maalum za SMZ, kwa namna ya kipekee alivyoiwezesha Ofisi yake hii kutekeleza mipango thabiti na madhubuti ikiwemo kuziimarisha kwa kila namna Idara Maalum za SMZ zikiwa sehemu ya vyombo vya ulinzi na usalama na yeye akiwa ndie Kamanda Mkuu. Hakika, ameweka historia muhimu katika kuziheshimisha, kuziimarisha na kuziwezesha Idara Maalum za SMZ.

6. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Ofisi hii imewezeshwa kutekeleza miradi zaidi ya 72 ikiwemo miradi ya kimkakati ya ujenzi wa masoko ya kisasa, mradi wa kuimarisha ulinzi na usalama, pamoja na mradi wa ujenzi wa Ofisi za Masheha ambapo imewezesha kuimarisha uchumi wa nchi yetu na kuimarika kwa ulinzi, usalama na utawala bora.

7. **Mheshimiwa Spika,** kwa dhati nikishukuru Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kuendelea kuwa chama madhubuti chenye sera imara na ilani inayotekelezeka kwa maslahi mapana ya nchi yetu na wananchi.

8. **Mheshimiwa Spika,** namshukuru Mheshimiwa Othman Masoud Othman Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kwa mashirikiano yake anayotupatia katika kuendeleza majukumu ya Ofisi hii. Aidha, kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar akiwa Mtendaji Mkuu wa shughuli za Serikali kwa maono yake na ukaribu wake katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii. Hakika amekua nguzo imara katika kutimiza mipango na malengo yaliyoelekezwa kutekelezwa na Ofisi.

9. **Mheshimiwa Spika,** natumia fursa hii kukushukuru na kukupongeza wewe kwa umahiri, uweledi na ujasiri wa kuliongoza Baraza hili Tukufu kwa hekima, busara na maono makubwa. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa anavyoendelea kusaidia kuliongoza Baraza hili kwa umakini. Kadhalika, nawapongeza Wenyeviti wa Baraza Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Dimani na Mheshimiwa Abdalla Hussein Kombo Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Mkoani kwa umahiri wao mkubwa wa kuendesha vikao vya Baraza la Wawakilishi. Vilevile, namshukuru na kumpongeza Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndugu Raya Issa Mselem kwa mashirikiano makubwa anayotupatia.

10. **Mheshimiwa Spika,** natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Machano Othman Said Mwakilishi wa Wananchi jimbo la Mfenesini kwa kuiongoza Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa hekima, busara na uadilifu. Kwa kipindi cha miaka mitano cha uongozi wake amekuwa nguzo imara na kiongozi wa kupigiwa mfano na kuwa ni chachu ya mafanikio yanayopatikana katika Ofisi yetu hii.

11. **Mheshimiwa Spika,** shukurani na pongezi pia ziwaendee Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Maryam Thani Juma Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Gando, Wajumbe wa Kamati Mheshimiwa Mussa Foum Mussa Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Kiwani, Mheshimiwa Abdalla Abass Wadi Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Nungwi, Mheshimiwa Haji Shaaban Waziri Mwakilishi wa Wananchi jimbo la Uzini, Mheshimiwa Suleiman Haroub Suleiman Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Kiembe Samaki, Mheshimiwa Jamal Kassim Ali Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Magomeni na Mheshimiwa Zaina Abdalla Salim Mwakilishi viti maalum Mkoa wa Magharibi kichama. Aidha, nawashukuru Makatibu wa Kamati Ndugu Ali Alawy

Ali, Ndugu Mwanaisha Moh'd Kheir, Ndugu Shawana Moh'd Haji na msaidizi wa Mjumbe wa Kamati Ndugu Amina Abeid Hemed kwa mashirikiano makubwa waliyotupatia. Kwa hakika hatuna cha kuilipa kamati hii isipokuwa tunawatakia kila la kheri Wajumbe wote na kuwaombea dua njema kwa Mwenyezi Mungu.

12. **Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi huo uliombatana na shukurani na pongezi, naomba uniruhusu sasa kuwasilisha hotuba yangu ya makadirio ya mapato na matumizi ya Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

## B. MAPITIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### Mapato ya Mfuko Mkuu wa Serikali

13. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ iliidhinishiwa kukusanya Shilingi **5,109,682,000** kupitia mafungu yake ya bajeti D01- D12 kwa ajili ya kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali. Hadi kufikia Machi 31/2025 Ofisi imefanikiwa kukusanya Shilingi **3,126,961,593** sawa na asilimia 61. (**Kiambatanisho nambari 1).**

### Upatikanaji wa jumla wa fedha za matumizi

14. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 nililiomba Baraza lako kuidhinisha Shilingi **350,012,745,000** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo za Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Hadi kufikia Machi 2025, Ofisi imeingiziwa Shilingi **233,045,760,067** sawa na asilimia 66 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo Shilingi 138,620,580,756 sawa na asilimia 95 zimetumika kulipa mishahara, Shilingi 18,390,247,752 sawa na asilimia 53 zilitumika kwa matumizi mengineyo,

Shilingi 13,459,134,671 sawa na asilimia 64 zimetumika kuzipatia ruzuku Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakala wa Ulinzi JKU na Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ na Shilingi 62,575,796,888 sawa na asilimia 42 zilitumika kwa kazi za maendeleo. **(Kiambatanisho nambari 2 na 3).**

**Upatikanaji wa Fedha kwa Kila Fungu (D01-D12)**

15. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Makao Makuu (Fungu D01) iliidhinishiwa matumizi ya Shilingi 97,269,016,000. Hadi kufikia Machi 2025, Shilingi 46,116,213,101 zimepatikana sawa na asilimia 47 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, Shilingi 1,679,109,112 sawa na asilimia 74 zilitumika kwa kulipa mishahara, Shilingi 1,413,840,178 sawa na asilimia 30 zilitumika kwa matumizi mengineyo, Shilingi 42,969,318,811 sawa na asilimia 48 zilitumika kwa kazi za maendeleo na Shilingi 53,945,000 sawa na asilimia 36 zilitumika kwa ruzuku ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ.

16. **Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Kujenga Uchumi (Fungu D02) liliidhinishiwa matumizi ya Shilingi 45,446,600,000. Hadi kufikia Machi 2025, limeingiziwa Shilingi 38,373,168,427 sawa na asilimia 84 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo Shilingi 32,618,492,855 sawa na asilimia 96 zilitumika kulipa mishahara, Shilingi 3,985,775,572 sawa na asilimia 52 zilitumika kwa matumizi mengineyo, Shilingi 128,900,000 sawa na asilimia 24 zilitumika kwa ruzuku ya Wakala wa Ulinzi wa JKU na Shilingi 1,640,000,000 sawa na asilimia 52 zilitumika kwa kazi za maendeleo. Aidha, Jeshi la Kujenga Uchumi liliidhinishiwa mapato ya Shilingi 2,242,633,000 kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali na kufanikiwa kukusanya mapato ya Shilingi 980,998,401 sawa na asilimia 44 ya makadirio ya mwaka. Kati ya Fedha hizo Shilingi 142,500,000 sawa na asilimia 99.9 zilikusanywa na JKU na Shilingi 838,498,401 sawa na asilimia 40 zilikusanywa na Wakala wa Ulinzi JKU.

17. **Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Mafunzo (Fungu D03) kiliidhinishiwa matumizi ya Shilingi 29,880,030,000. Hadi kufikia Machi 2025 kiliingiziwa Shilingi 26,598,237,577 sawa na asilimia 89 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo Shilingi 22,102,614,939 sawa na asilimia 98 zilitumika kulipa mishahara, Shilingi 4,195,622,638 sawa na asilimia 88 zilitumika kwa matumizi mengineyo na Shilingi 300,000,000 sawa na asilimia 12 zilitumika kwa kazi za maendeleo. Aidha, Chuo cha Mafunzo kiliidhinishiwa mapato ya Shilingi 173,600,000 kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali na kufanikiwa kukusanya mapato ya Shilingi 175,889,525 sawa na asilimia 101 ya makadirio ya mwaka.

18. **Mheshimiwa Spika,** Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (Fungu D04) kiliidhinishiwa matumizi ya Shilingi 44,584,040,000. Hadi kufikia Machi 2025 kiliingiziwa Shilingi 35,959,222,956 sawa na asilimia 81 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo Shilingi 32,915,615,233 sawa na asilimia 94 zilitumika kulipa mishahara, Shilingi 2,443,607,723 sawa na asilimia 55 zilitumika kwa matumizi mengineyo na Shilingi 600,000,000 sawa na asilimia 12 zilitumika kwa kazi za maendeleo. Aidha, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kiliidhinishiwa mapato ya Shilingi 94,230,000 kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali na kufanikiwa kukusanya mapato ya Shilingi 70,762,500 sawa na asilimia 75 ya makadirio ya mwaka.

19. **Mheshimiwa Spika,** Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (Fungu D05) kiliidhinishiwa matumizi ya Shilingi 58,207,259,000. Hadi kufikia Machi 2025 kiliingiziwa Shilingi 28,011,777,302 sawa na asilimia 48 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo Shilingi 17,292,571,696 sawa na asilimia 100 zilitumika kulipa mishahara, Shilingi 2,275,199,690 sawa na asilimia 63 zilitumika kwa matumizi mengineyo na Shilingi 8,444,005,916 sawa na asilimia 23 zilitumika kwa kazi za maendeleo. Aidha, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kiliidhinishiwa kukusanya mapato ya

Shilingi 153,747,000 kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali na kufanikiwa kukusanya mapato ya Shilingi 101,987,820 sawa na asilimia 66 ya makadirio ya mwaka.

20. **Mheshimiwa Spika,** Kikosi cha Valantia Zanzibar (Fungu D06) kiliidhinishiwa matumizi ya Shilingi 34,384,300,000. Hadi kufikia Machi 2025 kiliingiziwa Shilingi 33,214,266,536 sawa na asilimia 97 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo Shilingi 23,005,831,209 sawa na asilimia 102 zilitumika kulipa mishahara, Shilingi 1,971,992,666 sawa na asilimia 63 zilitumika kwa matumizi mengineyo na Shilingi 8,236,442,661 sawa na asilimia 94 zilitumika kwa kazi za maendeleo.

21. **Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa Mjini Magharibi (Fungu D07) uliidhinishiwa matumizi ya Shilingi 13,161,800,000. Hadi kufikia Machi 2025 uliingiziwa Shilingi 8,070,600,675 sawa na asilimia 60 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo Shilingi 1,821,377,153 sawa na asilimia 70 zilitumika kulipa mishahara, Shilingi 317,176,333 sawa na asilimia 21 zilitumika kwa matumizi mengineyo na Shilingi 5,932,047,189 sawa na asilimia 66 zilitumika kuyapatia ruzuku Mabaraza ya Manispaa na Baraza la Jiji. Aidha, Mkoa wa Mjini Magharibi uliidhinishiwa kukusanya mapato ya Shilingi 54,600,000 kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali na kuweza kukusanya mapato ya Shilingi 21,760,000 sawa na asilimia 40 ya makadirio ya mwaka. Kwa upande wa Mabaraza ya Manispaa Mjini, Magharibi 'A' na Magharibi 'B' yaliidhinishiwa kukusanya mapato ya ndani Shilingi 9,392,823,400 na kufanikiwa kukusanya Shilingi 4,809,598,273 sawa na asilimia 76 kwa makadirio ya miezi tisa na asilimia 51 kwa makadirio ya mwaka.

22. **Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa Kusini Unguja (Fungu D08) liliidhinishiwa matumizi ya Shilingi 4,294,600,000. Hadi kufikia Machi 2025 uliingiziwa Shilingi 2,060,379,261

sawa na asilimia 48 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo Shilingi 1,370,861,046 sawa na asilimia 67 zilitumika kulipa mishahara, Shilingi 181,359,862 sawa na asilimia 33 zilitumika kwa matumizi mengineyo na Shilingi 1,177,703,468 sawa na asilimia 70 zilitumika kwa ruzuku za Baraza la Mji Kati na Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja. Aidha, Mkoa wa Kusini Unguja uliidhinishiwa kukusanya mapato ya Shilingi 57,035,000 kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali na kuweza kukusanya mapato ya Shilingi 13,970,000 sawa na asilimia 24 ya makadirio ya mwaka. Kwa upande wa Baraza la Mji Kati na Halmashauri ya Wilaya ya Kusini waliidhinishiwa kukusanya mapato ya ndani Shilingi 2,723,712,800 na kufanikiwa kukusanya mapato ya Shilingi 1,737,131,635 sawa na asilimia 100 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 64 ya makadirio ya mwaka.

23. **Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa Kaskazini Unguja (Fungu D09) uliidhinishiwa matumizi ya shilingi 5,266,600,000. Hadi kufikia Machi 2025 uliingiziwa Shilingi 3,486,699,026 sawa na asilimia 66 kwa makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo Shilingi 1,465,570,705 sawa na asilimia 72 zilitumika kulipa mishahara, Shilingi 226,494,632 sawa na asilimia 30 zilitumika kwa matumizi mengineyo na Shilingi 1,794,633,689 sawa na asilimia 73 zilitumika kwa ruzuku za Baraza la Manispaa Kaskazini A na Baraza la Mji Kaskazini B . Aidha, Mkoa wa Kaskazini Unguja uliidhinishiwa mapato ya Shilingi 37,553,000 kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali na kuweza kukusanya Shilingi 5,510,000 sawa na asilimia 15 ya makadirio ya mwaka. Kwa upande wa Baraza la Manispaa Kaskazini 'A' na Baraza la Mji Kaskazini 'B' yaliidhinishiwa kukusanya mapato ya ndani Shilingi 4,480,101,950 na kuweza kukusanya Shilingi 2,470,704,238 sawa na asilimia 76 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 55 ya makadirio ya mwaka.

24. **Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa Kusini Pemba (Fungu D10) uliidhinishiwa matumizi ya Shilingi 5,859,000,000. Hadi kufikia Machi 2025 uliingiziwa Shilingi 4,364,867,653 sawa na asilimia 74 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo Shilingi 1,129,143,541 sawa na asilimia 74 zilitumika kulipa mishahara, Shilingi 280,213,834 sawa na asilimia 32 zilitumika kwa matumizi mengineyo na Shilingi 2,955,510,278 sawa na asilimia 86 zilitumika kwa ruzuku za Baraza la Manispaa ya Chake Chake na Baraza la Mji Mkoani. Aidha, Mkoa wa Kusini Pemba uliidhinishiwa kukusanya mapato ya Shilingi 47,116,000 kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali na kukusanya Shilingi 7,633,099 sawa na asilimia 16 ya makadirio ya mwaka. Kwa upande wa Baraza la Manispaa Chake Chake na Baraza la Mji Mkoani yaliidhinishiwa kukusanya mapato ya ndani shilingi 1,427,863,000 na kuweza kukusanya Shilingi 784,793,055 sawa na asilimia 70 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 55 ya makadirio ya mwaka.

25. **Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa Kaskazini Pemba (Fungu D11) uliidhinishiwa matumizi ya Shilingi 5,012,700,000. Hadi kufikia Machi 2025 uliingiziwa Shilingi 2,754,367,564 sawa na asilimia 55 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo Shilingi 1,096,055,517 sawa na asilimia 73 zilitumika kulipa mishahara, Shilingi 241,917,000 sawa na asilimia 26 zilitumika kwa matumizi mengineyo na Shilingi 1,416,395,047 sawa na asilimia 55 zilitumika kwa ruzuku za Baraza la Mji Wete na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni. Kwa upande wa Baraza la Mji Wete na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni walipangiwa kukusanya mapato ya ndani Shilingi 920,000,000 na kukusanya Shilingi 539,932,479 sawa na asilimia 59 ya makadirio ya mwaka na asilimia 80 ya makadirio ya miezi tisa.

26. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (Fungu D12) uliidhinishiwa matumizi ya

Shilingi 6,646,800,000. Hadi kufikia Machi 2025 uliingiziwa Shilingi 3,366,414,874 sawa na asilimia 51 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo Shilingi 2,123,337,750 sawa na asilimia 74 zilitumika kwa mishahara, Shilingi 857,047,624 sawa na asilimia 46 zilitumika kwa matumizi mengineyo na Shilingi 386,029,500 sawa na asilimia 20 zilitumika kwa miradi ya maendeleo. Aidha, Wakala uliidhinishiwa kukusanya mapato ya Shilingi 2,231,810,000 kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali na kufanikiwa kukusanya Shilingi 1,747,450,248 sawa na asilimia 78 ya makadirio ya mwaka.

## C. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA PROGRAMU ZA IDARA ZA MAKAO MAKUU YA AFISI (D01)

27. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, jumla ya malengo 13 yalipangwa kutekelezwa na Idara za Makao Makuu ya Ofisi ambapo utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

**1) Kuendelea kutekeleza Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama Zanzibar.**

28. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeanza kutekeleza shughuli zote zilizopangwa katika Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama. Miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa ni kuimarisha uwezo wa kijeshi wa Idara Maalum za SMZ kwa kuzipatia vifaa vya kijeshi vya kisasa, mifumo ya mawasiliano ya ulinzi na vitendea kazi. Utekelezaji wa Mradi huu umechangia usalama wa Zanzibar kwa kuhakikisha vitendo vya kihalifu na vya uvunjifu wa amani na utulivu vinadhibitiwa.

**2) Kuanza Ujenzi wa Mradi wa Kituo cha Mabasi ya Kisasa na Maegesho katika eneo la Bwawa la Mwanakwerekwe.**

29. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imekamilisha maandalizi na taratibu zote za Ujenzi wa Kituo cha Mabasi ya Kisasa na Maegesho katika eneo la bwawa la Mwanakwerekwe. Taratibu

hizo ni pamoja na kumpata mshauri elekezi na mkandarasi wa ujenzi. Hatua iliyopo sasa ni kuwasilisha mikataba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili ujenzi uanze kutekelezwa rasmi. Mradi huu unalenga kuwarahisisishia wananchi wa Zanzibar kupata huduma bora za usafiri, kuchochea fursa za kiuchumi na kuleta haiba na maendeleo endelevu ya Mji wetu.

**3) Kuanza ujenzi wa Chuo cha Mafunzo cha Kisasa Hanyegwa Mchana.**

30. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imefanikiwa kukamilisha taratibu za ujenzi wa Chuo cha Mafunzo kipya cha kisasa huko Hanyegwa Mchana. Mshauri elekezi aliyepatikana ni Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) na Mkandarasi wa ujenzi ni Kampuni ya Ujenzi ya Chuo cha Mafunzo ambapo hatua za awali za ujenzi zimeshaanza. Mradi huu unalenga kuimarisha Mfumo wa Haki Jinai nchini na ndani ya Chuo cha Mafunzo ikiwemo kuweka mazingira bora kwa Wanafunzi na Mahabusu.

**4) Kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Masheha.**

31. **Mheshimwa Spika,** Ofisi imesimamia ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Masheha ambapo jumla ya Ofisi 64 zimekamilika na kukabidhiwa ambapo baadhi zimeanza kutoa huduma kwa wananchi wa Shehia husika. Zoezi la kukabidhi ofisi hizo 64 kwa Masheha husika lilifanyika tarehe 10/04/2025 katika Shehia ya Matetema Wilaya ya Kaskazini "B" Mkoa wa Kaskazini Unguja. Ofisi hizi pia zimewekewa vitendea kazi ikiwemo samani (furnitures) na kompyuta. Kujengwa kwa ofisi hizi za Masheha kunachangia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za Serikali karibu na wananchi.

**5) Uzinduzi wa Masoko ya Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini.**

32. **Mheshimiwa Spika,** tuliahidi kuyazindua na kuyatumia masoko ya Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini ambapo utekelezaji wake umefanyika mwezi Oktoba, 2024 kwa Masoko ya Mwanakwerekwe na Jumbi. Masoko hayo yalizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na yameanza kutumika kuanzia mwezi wa Disemba 2024. Masoko hayo yameleta faida nyingi kama vile kupatikana maeneo mazuri na salama ya kufanyia shughuli za biashara na ujasiriamali kwa wananchi, kutoa nafasi kwa wakulima na wafanyabiashara wadogo na wakubwa kuuza bidhaa zao, fursa za ajira kwa vijana, wazee na wanawake na kutoa fursa kwa wananchi na wageni kupata vyakula bora na salama.

**6) Kufanya Ukarabati Mkubwa wa jengo la Ofisi kuu Pemba.**

33. **Mheshimwa Spika,** tumefanikiwa kufanya ukarabati mkubwa wa jengo la Ofisi kuu Pemba ambalo lilikuwa chakavu. Ukarabati huo umekamilika Mwezi Novemba 2024. Kufanyika kwa ukarabati kumehakikisha usalama wa Watumishi na Wananchi wanaofika Ofisini kupata huduma na umeboresha ufanisi wa kazi kwa kutoa mazingira bora zaidi.

**7) Utekelezaji wa Mradi wa Kijani Pemba.**

34. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imesimamia utekelezaji wa Mradi wa Kijani Pemba unaotekelezwa na Jumuiya ya OIKOS kwa Miji ya Wete na Micheweni na Jumuiya ya LVIA kwa Miji ya Chake Chake na Mkoani. Kazi zilizotekelezwa na mradi hadi kufikia Machi 2025 ni uwekaji wa umeme wa jua (Solar panels) katika visima vya ZAWA vilivyopo Kizimbani na Limbani Wete, ukarabati wa vyoo vya Skuli ya Miti Ulaya Wete na Skuli ya Madungu Msingi Chake Chake, mafunzo

maalum ya uchukuaji wa mikopo, uhifadhi wa fedha za mtaji, urudishaji wa mkopo na uwekaji wa akiba yametolewa kwa Wajasiriamali 150 kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba na wajasiariamali 150 kwa Mkoa wa Kusini Pemba. Mradi huu unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya unalenga kupunguza umasikini na kukuza maendeleo endelevu kwa wananchi wa Wete, Micheweni, Mkoani na Chake Chake.

**8) Kuzipatia Serikali za Mitaa Vifaa vya Kisasa vya Usafi.**

35. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeagiza magari ya kisasa 29 ambapo yatakapowasili nchini yatagaiwa katika Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri zote za Unguja na Pemba ili kuziwezesha kutekeleza jukumu lao la msingi la usimamizi wa usafi wa mazingira. Napenda kulitaarifu Baraza lako kwamba Ofisi imefanikiwa kuanza kupokea magari mawili ya kisasa yenye uwezo wa kubeba makontena makubwa ya kuhifadhia taka na kuzipeleka Jaa kuu la Kibele pamoja na kupokea makontena 30 ya kisasa ya kuhifadhia taka. Aidha, Ofisi inatarajia kupokea magari mengine yaliyobakia ndani ya mwaka huu 2025.

**9) Maendeleo ya Jumuiya Zisizo za Kiserikali (NGOs) Zanzibar.**

36. **Mheshimiwa Mweyekiti,** Serikali imeendelea kuthamini juhudi zinazochukuliwa na Jumuiya zisizo za Kiserikali (NGOs) katika kusaidia maendeleo ya jamii na kukuza uchumi wetu. Katika kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa, Afisi ya Mrajis wa Jumuiya zisizo za Kiserikali Zanzibar imeendelea kutekeleza kazi za usajili, uratibu, ufuatiliaji na usimamizi wa NGOs kwa kuhakikisha kuwa Jumuiya hizo zinafanya kazi zao kwa uweledi na kufuata Sheria za nchi. Kadhalika, Ofisi imefanikiwa kufanya Mkutano Mkuu wa NGOs Zanzibar uliofanyika tarehe 25/02/2025 katika Ukumbi wa Dkt. Ali Mohammed Shein Tunguu-SUZA ambapo jumla ya NGOs 844 ziliweza kushiriki.

37. **Mheshimiwa Spika,** mchango wa NGOs katika kusaidia maendeleo ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2024/2025 umeongezeka kwa asilimia 68 ikilinganishwa na mwaka 2023/2024. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya Shilingi 79,656,297,914.07 zilitumiwa na NGOs 196 kwa mujibu wa ripoti zao za kifedha. Kati ya fedha hizo, jumla ya Shilingi 61,410,223,442 zilitumiwa na NGOs 178 za Unguja na Shilingi 8,625,547,892 zilitumiwa na NGOs 18 za Pemba. Sehemu ya fedha hizo zimetumika katika utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo kwa wananchi wa mijini na vijijini **(Kiambatanisho nambari 4).**

**10) Kuboresha maendeleo ya Viwanda vya Idara Maalum za SMZ.**

38. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeendelea kuboresha maendeleo ya Viwanda vya Idara Maalum za SMZ vilivyopo Makao Makuu ya KVZ Mtoni. Viwanda vimeboreshwa kwa kupatiwa mashine mpya 13, malighafi ya ngozi za viatu, malighafi za kutengeza mifuko isiyo ya plastiki, malighafi za machapisho mbali mbali ya mabango, fulana, bendera na vitambaa vya kushonea sare za Idara Maalum za SMZ. Vile vile, viwanda vimepatiwa vifaa mbali mbali vya ushoni wa viatu na nguo kwa lengo la kuhakikisha vinazalisha mahitaji ya Idara Maalum za SMZ na mahitaji ya wananchi wanaohitaji huduma za Viwanda hivyo. Aidha, Viwanda vimewekewa mifumo ya TEHAMA ili kuhakikisha huduma zake zinatolewa kwa njia ya kidijitali.

**11) Kuimarisha Mfumo wa Mafunzo wa Idara Maalum za SMZ.**

39. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imefanikiwa kuimarisha mfumo wa mafunzo wa Idara Maalum za SMZ. Mafunzo endelevu kwa Maafisa na Wapiganaji yametolewa ambayo yamewajengea

uwezo wa kukabiliana na hali mbali mbali za kiusalama. Mafunzo hayo yalijumuisha masuala ya maadili, sheria za kiusalama na mbinu bora za kushughulikia migogoro ya kiusalama na kiulinzi. Pia, mafunzo ya Afisa Kadeti yametolewa na kuendelea kuratibiwa kwa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) na Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ). Aidha, kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama Ofisi imefanikiwa kuratibu mafunzo maalum ambayo yamepelekea uratibu mzuri wa operesheni za kiulinzi kwa lengo la kuweka usalama bora zaidi wa wananchi na mali zao.

**12) Upandishaji hadhi Halmashauri ya Wilaya ya Kusini na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.**

40. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imekamilisha taratibu za kufanya tathmini ya kina ambayo imezingatia matakwa ya Sheria nambari 07 ya mwaka 2014, Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kupandisha hadhi Serikali za Mitaa. Afisi iliahidi kuanzisha mchakato wa upandishwaji hadhi wa Halmashauri mbili za Wilaya ya Kusini na Wilaya ya Micheweni, hata hivyo mchakato huo ulijumuisha pia Mabaraza ya Miji Kati na Kaskazini 'B'. Kwa kuzingatia tathmini iliyofanyika, Ofisi iliwasilisha ripoti na mapendekezo yake Serikalini kwa hatua stahiki.

41. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba Serikali imeridhia na kupandisha hadhi Baraza la Mji Kati kuwa Manispaa na Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kuwa Baraza la Mji. Hatua nyengine zinazofuata za utekelezaji wa maamuzi hayo ya Serikali zitaanza katika mwaka wa fedha 2025/2026.

## D. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ

42. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Idara Maalum za SMZ zilipanga kutekeleza malengo makuu 17 ambapo utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

## 1) Kuimarisha Mazingira ya Kazi na Makaazi ya Maafisa na Wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ

a. Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimefanikiwa kujenga mahanga na afisi katika Kambi ya Kizimkazi, kimejenga jengo la Afisi ya ghorofa moja katika Kambi ya Bwefum na kimejenga Bwalo la maafisa la ghorofa moja katika Kambi ya Wete. Majengo yote hayo yamefunguliwa rasmi mwezi wa Januari 2025 na yameanza kutoa huduma kwa Maafisa na Wapiganaji wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo. Aidha, Kikosi kupitia vyanzo vya ndani vya mapato kimefanikiwa kununua gari tano kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Kikosi.

b. Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) limekamilisha ujenzi wa Jengo la Ofisi Kuu ya JKU Wawi la ghorofa moja. Kadhalika JKU imeendeleza ujenzi wa mahanga ya kisasa ya ghorofa moja katika eneo la Ng'ambwa Gombani Pemba ambapo ujenzi wake umefika asilimia 50. JKU pia imekamilisha taratibu za kuanza ujenzi wa dahalia kwa ajili ya wanafunzi wa Skuli ya Sekondari JKU na Skuli ya Ufundi JKU Mtoni. Aidha, JKU kupitia mapato yake ya ndani imejenga Kituo cha Mafuta katika eneo lake la Mtoni na kufanya ukarabati wa baadhi ya majengo yake katika Kambi zake.

c. Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU) kimefanikiwa kuanza na kukamilisha ujenzi wa Vituo vya Zimamoto na Uokozi katika Shehia ya Mkanyageni Pemba Wilaya ya Mkoani na Shehia ya Kiwegwa Wilaya ya Kaskazini 'B'. Aidha, Kikosi kimeanza ujenzi wa Vituo vya Zimamoto na Uokozi Kibuteni na Bwejuu pamoja na ujenzi wa Hanga Mkanyageni Pemba. Vilevile, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kupitia vyanzo vyake vya ndani vya mapato kimefanya ujenzi wa Chuo cha Maafisa wa Zimamoto na Uokozi Buyu na kuanza maandalizi ya ujenzi wa vituo vyengine vya zimamoto na uokozi kwa Unguja na Pemba.

d. Chuo cha Mafunzo kimekamilisha ujenzi wa Jengo la Mkao Makuu ya Chuo cha Mafunzo Kilimani lenye ghorofa nne ambalo limefunguliwa mwezi Januari 2025 na kwa sasa linatoa huduma. Aidha, Chuo Cha Mafunzo kimeanza na kuendelea na ujenzi wa mahanga katika Kambi za Hanyegwa Mchana na Bumbwini.Vilevile, kupitia vyanzo vyake vya ndani vya mapato kimeanza ujenzi wa mahanga mawili katika kambi ya Kangagani.

e. Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ) kimefanikiwa kufanya ujenzi wa mahanga 10 katika Kambi za Pangatupu, Micheweni, Pujini, Kikungwi na Mwanyanya pamoja na kuanza kujenga majengo ya Ofisi ya ghorofa moja katika Kambi za Kiashange na Pujini. Vilevile, KVZ imejenga uzio wa Kambi zake Micheweni na Ndugukitu Pemba. Aidha, Kikosi cha Valantia Zanzibar kupitia vyanzo vyake vya ndani vya mapato kimenunua gari 6 kwa matumizi mbali mbali ya Kikosi.

**2) Kuimarisha Huduma za Zimamoto na Uokozi Zanzibar.**

43. **Mheshimiwa Spika,** Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimefanikiwa kuimarisha huduma za Zimamoto na Uokozi kwa lengo la kuhakikisha usalama wa wananchi, wageni, wawekezaji na mali zao. Huduma hizo zimehusisha mifumo bora ya majibu ya dharura kupitia namba 114, ununuzi wa vifaa vya kisasa pamoja na kuboresha mafunzo kwa Maafisa na Wapiganaji wa Zimamoto na Uokozi. Katika matukio ya moto yaliyoripotiwa, Kikosi kimefanikiwa kuwaokoa watu 58 wakiwa hai pamoja na kuokoa mali za wananchi waliopatwa na majanga ya moto zenye thamani ya Shilingi 15,985,727,500 kwa makisio.

**3) Kusimamia Upatikanaji wa Magari, Boti na Vifaa vya Zimamoto**.

44. **Mheshimiwa Spika,** Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU) kimefanikiwa kukamilisha taratibu zote na kufunga mkataba

wa kupatiwa magari 27, boti moja na vifaa mbalimbali vya zimamoto na uokozi kwa njia ya mkopo nafuu kutoka Serikali ya Austria. Malipo ya asilimia 30 yamelipwa kwa Mzabuni husika ambapo kuanzia mwezi wa Julai 2025, Kikosi kitapokea gari sita za aina ya "rapid vehicles", boti ya kisasa ya zimamoto pamoja na pampo za kuzimia moto. Aidha, gari zilizobakia zinategemea kuwasili nchini kuanzia mwezi wa Novemba 2025.

**4) Kuimarisha Ulinzi wa Mipaka ya Bahari ya Zanzibar**

45. **Mheshimiwa Spika,** Ulinzi wa mipaka ya bahari ni muhimu kwa usalama wa Taifa, biashara na rasilimali za nchi yetu. Katika kuboresha ulinzi huo, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimeendesha mafunzo maalum ya operesheni za Kijeshi baharini kwa lengo la kuhakikisha Maafisa na Wapiganaji wake wana uwezo wa kukabiliana na matukio mbalimbali yanayotokea baharini. Kikosi kimetumia mfumo wa kufuatilia mwenendo na shughuli zote zinazofanywa na vyombo vyote vinavyoingia kwenye bahari ya Zanzibar kwa kushirikiana na Kikosi cha Wanamaji wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) pamoja na Mamlaka za Usafiri wa baharini ikiwemo ZMA. Vilevile, Kikosi kimefunga mkataba wa kupeleka boti chelezoni ili kuhakikisha boti hizo zinakuwa imara muda wote. Aidha, KMKM imefanikiwa kukabiliana na changamoto za usalama baharini kwa kupambana na uharamia na biashara haramu ambapo jumla ya matukio ya magendo 49 yamekamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

**5) Kuimarisha Mfumo wa Haki Jinai Chuo cha Mafunzo**

46. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha huduma za urekebishaji tabia na kuhakikisha haki za wanafunzi na mahabusu zinaheshimiwa, Chuo cha Mafunzo kimechukuwa hatua mbalimbali kwa lengo la kuimarisha haki jinai kwa wanafunzi na mahabusu nchini. Chuo Cha Mafunzo

kimetowa huduma za kielimu na kisaikolojia kwa Wanafunzi na Mahabusu ili kuwasaidia kujifunza stadi mpya na kuwa tayari na maisha baada ya kumaliza na kutoka Chuo cha Mafunzo. Kadhalika, Chuo Cha Mafunzo kimefanya mapitio na kuja na mapendekezo ya mitaala mipya ya urekebishaji tabia kwa Wanafunzi na Mahabusu. Chuo kimepokea na kuwapa huduma zote za kibinadamu Wanafunzi na Mahabusu. Pia, jumla ya wanafunzi 339 wameruhusiwa kutoka Chuo cha Mafunzo baada ya kumaliza muda wao wakiwemo 33 ambao walipata msamaha wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

**6) Kufanya Mageuzi ya Mafunzo ya Ujenzi wa Taifa**

47. **Mheshimiwa Spika,** Jeshi la kujenga Uchumi limefanikiwa kuweza kufanya mageuzi ya kutoa mafunzo ya ujenzi wa Taifa kwa lengo la kuimarisha uwezo wa vijana na jamii kwa ujumla. Mageuzi hayo yamehusisha kuboresha mbinu, maudhui na malengo ya mafunzo ili kuhakikisha kuwa yanakidhi mahitaji ya kisasa na changamoto zilizopo. Mafunzo ya Ujenzi wa Taifa yametolewa kwa vijana 8,505 ambayo yamezingatia malezi bora ya vijana kwa kuwafundisha uzalendo, historia na umuhimu wa amani na utulivu. Vijana hao wamepatiwa mafunzo ya uzalishaji mali kupitia sekta ya kilimo, mifugo, uvuvi na viwanda ili waweze kujiajiri. Aidha, mafunzo ya ufundi yanayotolewa na Skuli ya ufundi JKU yameboreshwa ambapo kwa sasa vijana hao wanatakiwa kujisajili katika mfumo wa elimu ya mafunzo ya amali na kutakiwa kufanya mitihani ya Kitaifa.

**7) Kuimarisha Operesheni za Ulinzi wa Raia na Mali zao.**

48. **Mheshimiwa Spika,** Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ), kimefanikiwa kuimarisha operesheni za kiulinzi kwa kushirikiana na vyombo vyengine vya ulinzi na usalama kwa lengo la kuhahakisha usalama wa wananchi na mali zao unaendelea kuwepo. Serikali imeendelea kukiimarisha

Kikosi cha Valantia ili kuendelea kulitekeleza jukumu la msingi la Ulinzi wa raia na mali zao kwa ufanisi zaidi. Kadhalika, Kikosi kimefanikiwa kufanya kazi kwa karibu na wananchi na kutoa huduma za ulinzi kwa majengo ya Serikali Unguja na Pemba.

**8) Kuboresha Huduma za Afya katika Idara Maalum za SMZ**

49. **Mheshimiwa Spika,** Idara Maalum za SMZ zimefanikiwa kuboresha huduma za afya zitolewazo kwenye makambi yake Unguja na Pemba. Lengo la maboresho hayo ni kuhakikisha Maafisa, Wapiganaji na wananchi wanawezeshwa kujikinga dhidi ya magonjwa mbalimbali, kupata matibabu na kuishi maisha bora. Katika kufanikisha lengo hilo, Idara Maalum za SMZ zimefanya maboresho yafuatayo;

a. Kikosi cha Valantia Zanzibar kimefanikiwa kuanza kujenga majengo ya kisasa ya Hospitali mbili katika Kambi za KVZ Mtoni Unguja na KVZ Ndugukitu Pemba pamoja na kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kambi ya Muyuni.

b. Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimefanikiwa kufanya manunuzi ya vifaa tiba vya kisasa na kuvisambaza katika Hospital yake ya KMKM Kibweni na Kituo cha Afya KMKM Gando kwa lengo la kutoa huduma bora za kiafya kwa maafisa, Wapiganaji na Wananchi.

c. Jeshi la kujenga Uchumi limefanya maboresho ya Hospital yake iliyopo Makao Makuu ya JKU Saateni kwa kununua vifaa tiba. Aidha, limenunuwa vitanda 80 vya wagonjwa na kuvisambaza katika Vituo vyake vya Afya Unguja na Pemba.

d. Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimeanza kutoa huduma za afya katika Kambi zake za Kilimani, Kitogani na Chanjaani Pemba ambapo Maafisa, Maaskari na Wananchi wanafika kupatiwa matibabu na ushauri wa kiafya.

e. Chuo cha Mafunzo kimeendelea kutoa huduma za afya katika Kituo chake cha Afya kilichopo Kilimani na kimeanza maandalizi ya Ujenzi wa Hospital ya Kisasa ya Chuo cha Mafunzo.

f. Kwa ujumla Idara Maalum zote za SMZ zimeongeza idadi ya wataalamu wa afya na zimepeleka masomoni madaktari wake kuongeza ujuzi katika vyuo mbali mbali nchini na nje ya nchi.

**9) Kulea na Kukuza Vipaji vya Wanamichezo**

50. **Mheshimiwa Spika,** Idara Maalum zote za SMZ zimefanikiwa kulea na kukuza vipaji vya wana michezo kwa lengo la kuhakikisha kwamba wana michezo wanapata fursa za kuonyesha uwezo wao na kuendeleza michezo nchini. Kwa muktadha huo, kuna hatua kadhaa zimeweza kuchukuliwa ikiwemo Jeshi la Kujenga Uchumi limeendeleza Kituo chake cha kulea vipaji vya wanamichezo wa mpira wa miguu kilichopo JKU Kama, ambacho kwa mwaka wa 2024/2025 kimefanikiwa kuwapeleka wanamichezo wawili kucheza kwa majaribio nchini Uturuki katika klabu ya Hatayspor na vijana wanne wamepandishwa kuichezea Timu ya JKU inayoshiriki Ligi Kuu ya Zanzibar. Kwa upande wa Kikosi cha Valantia Zanzibar kimepeleka wachezaji saba kuchezea klabu mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara. Aidha, timu zote za Idara Maalum za SMZ zimeendelea kushiriki katika mashindano mbalimbali yaliyoandaliwa nchini ambayo yametoa fursa kwa wanamichezo wa Idara Maalum za SMZ kuonyesha vipaji vyao.

**10) Kuzijengea Uwezo Kampuni za Ujenzi za Idara Maalum.**

51. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni za ujenzi za Idara Maalum za SMZ, zimejengewa uwezo ili ziweze kushindana katika soko la ndani na kimataifa. Uwezo huo umejumuisha kupatiwa Wataalam wa Uhandisi na kupatiwa mafunzo yaliyohusu mbinu bora za ujenzi na teknolojia zinazotumika

ulimwenguni kwa lengo la kuboresha ujuzi wa watendaji. Vile vile, Kampuni zimeweza kufanya kazi kwa kushirikiana na Wataalamu wa sekta mbalimbali kwa lengo la kuongeza uwezo wa kampuni katika kutekeza miradi mikubwa ya maendeleo. Aidha, Kampuni zimefanya mazungumzo na sekta za kifedha nchini ili kupata mikopo ya ununuzi wa zana na vifaa vya kisasa vya ujenzi.

**11) Kuandaa Miradi ya Maendeleo inayojiendesha (Bankable Projects)**

52. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza maagizo ya Serikali ya kupunguza utegemezi wa bajeti ya Serikali kuu, Idara Maalum za SMZ, zimeandaa miradi mbali mbali ya maendeleo inayojiendesha. Miongoni mwa miradi iliyoandaliwa na kuanza kutekelezwa ni miradi ya ujenzi wa vituo vya mafuta katika maeneo ya Kambi zao. Kwa mfano Jeshi la Kujenga Uchumi limejenga Kituo cha Mafuta katika eneo la Mtoni na Kikosi cha Valantia Zanzibar kimejenga Kituo cha mafuta katika Kambi yake ya KVZ Mtoni. Vituo hivi viwili vyote viliekewa mawe ya msingi katika maadhimisho ya sherehe za miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, vikosi vyengine vya KMKM, KZU na Chuo cha Mafunzo wameshaandaa miradi ya ujenzi wa vituo vya mafuta na hatua ya sasa ni kukamilisha taratibu za kimkataba.

**12) Kufanya Marekebisho ya Sheria za Idara Maalum za SMZ**

53. **Mheshimiwa Spika,** katika kikao kilichopita cha bajeti tuliahidi kufanya marekebisho ya sheria za Idara Malum za SMZ ili kuhakikisha kuwa sheria hizo zinaendana na mahitaji ya kisasa. Katika kufanya mapitio ya sheria hizo kazi zilizofanyika ni kufanya uchambuzi wa hitaji la marekebisho, kufanya utafiti na uchambuzi wa kina wa marekebisho yanayopendekezwa, kuandaa rasimu husika na kuziwasilisha rasimu hizo kwa Wadau kwa kupata maoni zaidi. Aidha, Sheria nambari 01 ya Mwaka 2003 ambayo ni

Sheria ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) na Sheria nambari 05 ya Mwaka 2004 ambayo ni Sheria ya Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ) ziliwasilishwa Barazani na kufanyiwa marekebisho kupitia mswada wa marekebisho ya sheria mbalimbali uliowasilishwa mwishoni mwa mwaka 2024. Sheria zilizobakia ikiwemo Sheria ya Tume ya Utumishi wa Idara Maalum za SMZ zipo katika hatua za mwisho za kuwasilishwa kwenye vikao vya Makatibu Wakuu na Baraza la Mapinduzi kwa taratibu.

**13) Kuyaboresha Maslahi ya Maafisa na Wapiganaji**

54. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imeboresha maslahi ya Maafisa na Wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ kwa lengo la kuwaongezea motisha. Vile vile, Serikali imewapatia mafunzo maafisa na wapiganaji ili waweze kuwa na uweledi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kiulinzi na kiusalama. Aidha, Serikali imewapandisha vyeo Maafisa 243 na Wapiganaji 1,435.**(Kiambatanisho nambari 5)**

**14) Kuendelea kuyapima na kuyapatia hati maeneo ya Idara Maalum za SMZ.**

55. **Mheshimiwa Spika,** Idara Maalum za SMZ zimeendelea na zoezi la kuyapima na kuyapatia hatimiliki maeneo yake kwa kushirikiana na Kamisheni ya Ardhi Zanzibar. Lengo la kupata hati za matumizi ya ardhi ni muhimu katika kuepusha migogoro na wananchi wanaozunguka maeneo ya Kambi. Hadi kufikia Machi 31, 2025 hati mpya zifuatazo zimeweza kupatikana;

a. Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimepatiwa hatimiliki kwa Kambi zake mbili ambazo ni Ukunjwi na Kiuyu Mbuyuni katika Mkoa wa Kaskazini Pemba.

b. Chuo cha Mafunzo kimefanikiwa kupata hatimiliki kwa Kambi ya Makao Makuu Kilimani, eneo la maduka ya Chuo cha Mafunzo Matumbaku na eneo la jengo lake lililopo Shehia ya Miembeni.

c. Jeshi la kujenga Uchumi limepatiwa hati ya Kambi za Kama, Dunga na Mtoni.

d. Kikosi cha Valantia Zanzibar kimepatiwa hati za Kambi ya Mtoni, Pujini, Kikungwi, Muyuni na Mto wa maji.

e. Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimepatiwa hati za Kambi zake za Makao Makuu Kilimani na Finya Wete.

## E. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA TAWALA ZA MIKOA

56. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2024/2025 jumla ya malengo makuu manane yalipangwa kutekelezwa na Tawala za Mikoa kupitia Ofisi za Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya ambapo utekelezaji wake ni kama ifuatavyo;

### 1) Kuanza taratibu za ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya Unguja na Pemba

57. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Ofisi za Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya zimekamilisha taratibu zote za maandalizi ya ujenzi wa Ofisi mpya za Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya Unguja na Pemba. Taratibu hizo zimejumuisha upatikanaji wa maeneo ya ujenzi wa Ofisi, michoro ya ujenzi husika na ithibati ya Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA).

Ujenzi rasmi wa Ofisi hizo unatarajiwa kuanza katika Mwaka wa fedha 2025/2026 kupitia bajeti ya ujenzi wa majengo ya Serikali inayosimamiwa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango **(Kiambatanisho nambari 6a na 6b).**

**2) Kudumisha amani, utulivu, umoja na mshikamano.**

58. **Mheshimiwa Spika,** Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya zina jukumu maalum la kuhakikisha usalama na utulivu wa nchi, raia na mali zao. Kamati hizo zimeweza kutatua masuala mbali ya kiusalama kupitia vikao 178 vilivyofanyika ambavyo vilijadili masuala ya kiusalama, ufuatiliaji wa sera na miongozo ya Serikali,uandishi wa daftari la wapiga kura wapya, hadhari ya majanga asilia, magonjwa na vitendo vya uhalifu vinavyoweza kutokea katika jamii pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Mikoa,Wilaya na Shehia.

59. **Mheshimiwa Spika,** Vikao hivyo vimesaidia si tu kupunguza uhalifu na vitendo vya uvunjifu wa amani bali pia vimeweza kuimarisha mahusiano kati ya Serikali na wananchi ambayo yameimarisha amani, utulivu, umoja na mashirikiano nchini.

**3) Kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kisekta katika Mikoa.**

60. **Mheshimiwa Spika,** kwa mafanikio makubwa Ofisi za Waheshimiwa Wakuu Mikoa na Wilaya zimesimamia utekelezaji wa Miradi ya maendeleo ya Serikali na Sekta binafsi inayotekelezwa ndani ya Mikoa yote ya Unguja na Pemba. Usimamizi huo umeihusisha Mikoa katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao kwa kushirikiana na Sekta husika. Miradi iliyosimamiwa imehusisha ujenzi wa miradi ya miundombinu, miradi ya afya, miradi ya elimu, miradi ya kilimo, miradi ya uwekezaji na miradi ya uhifadhi wa Mazingira. Naomba kuzipongeza sekta zote kwa mashirikiano makubwa waliyotupatia

ambayo yamewezesha Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya kusimamia miradi hiyo ya maendeleo kwa ustawi wa maisha ya wananchi na ukuzaji uchumi wa nchi yetu.

**4) Kusikiliza na kutatua changamoto mbalimbali za Wananchi.**

61. **Mheshimiwa Spika,** moja ya kazi kubwa inayofanywa na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na Waheshimiwa Masheha ni kusikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili wananchi katika maeneo yao kwa kushirikiana na sekta husika. Changamoto hizo zimejumuisha upatikanaji wa huduma za kijamii ikiwemo elimu, afya, maji na umeme, miundombinu ya barabara, masuala ya ajira na shida binafsi za wananchi. Hatua hii ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa maagizo ya Mheshimwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambae amekuwa akiwasisitiza Viongozi na Watendaji wote kusikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili wananchi.

**5) Kufanya suluhu ya migogoro ya ardhi kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi.**

62. **Mheshimiwa Spika,** Wananchi wameendelea kuzitumia Ofisi za Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kusuluhisha migogoro ya ardhi kwa lengo la kupata suluhu juu ya umiliki na matumizi ya ardhi. Jumla ya migogoro ya ardhi 160 ilipokelewa katika Ofisi za Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya, ambapo migogoro 90 imefanikiwa kupatiwa ufumbuzi kwa kushirikiana na Viongozi na Watendaji wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi. Aidha, migogoro iliyobakia inaendelea kufanyiwa kazi kwa kushirikiana na Wizara husika.**(Kiambatanisho namba 7)**

**6) Kufuatilia utekelezaji wa ahadi na maagizo ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa.**

63. **Mheshimiwa Spika,** Mikoa imefanikiwa kufuatilia utekelezaji wa ahadi na maagizo ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kufuatia ziara walizozifanya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwenye Mikoa na Wilaya husika. Ahadi na maagizo yanayotolewa na Viongozi wetu Wakuu katika ziara wanazofanya ni sehemu ya kuimarisha Utawala bora na kutatua changamoto za wananchi.

**7) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Mpango Mkuu wa Kupambana na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto.**

64. **Mheshimiwa Spika,** Mikoa imefanikiwa kutoa mafunzo ya uhifadhi wa mtoto kwa waratibu wa Shehia yenye lengo la kukuza uelewa juu ya kukabiliana na changamoto za udhalilishaji wa Wanawake na Watoto. Mikoa kwa kushirikiana na Shirika la kuwahudumia Watoto (Save the Children) imetoa mafunzo kwa Mabaraza ya Watoto ya Wilaya zote 11 juu ya kupinga vitendo ya ukatili na udhalilishaji wa watoto ikiwemo haki na wajibu kwa watoto.

65. **Mheshimiwa Spika,** Mikoa imefanikiwa kufanya zoezi la uhamasishaji wa kupinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji. Jumla ya wanafunzi 1,955 wa Skuli (wanawake 1,305 na wanaume 650), wanafunzi 986 wa Madrasa (wanawake 593 na wanaume 393) na wananchi 2,121 (wanawake 1,401 na wanaume 720) wameweza kufikiwa. Aidha, Mikoa na Wilaya imesimamia mikakati iliyojiekea kuunganisha nguvu za pamoja kati ya Ofisi za Mkoa, raia wema na askari wa ulinzi shirikishi katika Mikoa na Wilaya zake pamoja na kuimarisha mfumo wa mawasiliano baina ya vikosi kazi vilivyoundwa na uongozi wa Mikoa.

8) **Kuratibu na kusimamia shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa.**

66. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi za Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya zimesimamia Mabaraza ya Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri katika utekelezaji wa majukumu yao ya kutoa huduma kwa wananchi. Katika usimamizi huo, jumla ya vikao 28 vilifanyika ambavyo vilihusisha Viongozi na Watendaji wa Mikoa na Wilaya wakiwemo Waheshimiwa Madiwani na Waheshimiwa Masheha. Aidha, vikao vya Kamati ya Maendeleo (RDC) kwa kila Mkoa vilifanyika ambavyo pamoja na mambo mengine vilijadili utekelezaji wa mipango na bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

## F. MAFANIKIO YA PROGRAMU ZA USIMAMIZI WA SERIKALI ZA MITAA

67. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, jumla ya malengo 15 yalipangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

**1) Kuongeza kasi ya ukusanyaji mapato.**

68. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetekeleza jukumu lake la msingi la ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo mbali mbali kama vile ada za leseni, tozo za huduma na kodi za biashara. Jumla ya shilingi 10,328,229,430 zimekusanywa sawa na asilimia 79 kwa makadirio ya miezi tisa. Fedha hizo zimetumika kutekeleza shughuli za maendeleo na utoaji wa huduma kwa wananchi pamoja na uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**2) Kusimamia mikakati ya usafi wa mazingira katika miji.**

69. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za Serikali za Mitaa zimesimamia na kutekeleza mikakati ya kuimarisha usafi wa mazingira katika miji yetu ya Unguja na Pemba kwa lengo la kuzuia magonjwa kama vile kipindupindu na kuboresha hali ya maisha ya wananchi. Mikakati iliyotekelezwa imehusisha

ukusanyaji wa taka kwa njia sahihi na kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa usafi wa mazingira. Aidha, Mabaraza ya Manispaa, Miji na Halmashauri yamefanikiwa kuondosha tani zisizopungua 121,866 za taka zilizokusanywa katika Shehia za Unguja na Pemba.

**3) Kusimamia miundombinu ya masoko na maeneo ya wajasiriamali**

70. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za Serikali za Mitaa zimefanikiwa kusimamia miundombinu ya masoko na maeneo ya wajasiriamali ambayo yamejengwa katika Wilaya zote nchini ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kuwajengea Wajasiriamali maeneo maalum na ya kudumu ya kufanyia biashara zao. Usimamizi huo umehusisha kuwapanga Wajasiriamali ndani ya masoko ikiwemo Soko la Mwanakwerekwe na Soko la Jumbi, kuboresha hali ya usafi katika maeneo ya masoko na kukuza ushirikiano kati ya Serikali na Wajasiriamali ambao umeweza kutambua changamoto zilizopo kwenye masoko na kutafuta suluhisho la pamoja.

**4) Kuwasajili na kuwaendeleza Wajasiriamali wadogo.**

71. **Mheshimiwa Spika,** jitihada za kuwawezesha Wananchi kiuchumi kupitia makundi maalum ya Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu zimeendelea kufanyika. Jumla ya Shilingi 544,696,882 zimewasilishwa katika Mfuko wa pamoja katika Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwezeshaji ili kuyawezesha makundi hayo kupata huduma jumuishi za kifedha na kuweza kuendesha shughuli za ujasiriamali. Aidha, wajasiriamali 1,541 wamesajiliwa na kati yao, Wajasiriamali 952 tayari wamepatiwa vitambulisho baada ya kukamilisha taratibu za malipo.**(Kiambatanisho nambari 8)**

**5) Ujenzi wa masoko, bustani, viwanja vya kufurahishia Watoto, na vituo vya daladala.**

72. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutekeleza miradi ya maendeleo ziliahidi kujenga masoko, bustani, viwanja vya kufurahishia watoto, stendi na vituo vya daladala katika maeneo yao kupitia fedha za mapato ya ndani ambapo utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

a) Baraza la Manispaa Magharibi "A" limefanikiwa kukamilisha ujenzi wa Soko la Mtoni kwa Kisasi lenye uwezo wa kuchukua wajasiriamali 110 kwa wakati mmoja. Soko hilo lilifunguliwa Mwezi Januari, 2025 na limeanza kutoa huduma kwa wananchi.

b) Baraza la Manispaa Kaskazini "A" limekamilisha kujenga Soko la Mkwajuni ambalo limeweza kufunguliwa Mwezi Januari, 2025 likiwa na uwezo wa kuchukua wajasiriamali 400. Soko hili tayari limeanza kutoa huduma kwa wananchi.

c) Baraza la Manispaa Chake Chake limefanikiwa kuanza na kukamilisha kujenga Soko la Vitongoji na kufunguliwa rasmi mwezi Disemba, 2024. Soko hili lina uwezo wa kuchukua wajasiriamali 100 na kwa sasa limeanza kutoa huduma kwa wananchi. Vile vile, Baraza limekamilisha ujenzi wa Bustani ya Mwanamashungi ambayo imezinduliwa rasmi mwezi Januari, 2025.

d) Halmashauri ya Wilaya ya Kusini imekamilisha ujenzi wa kiwanja cha kufurahishia Watoto Paje ambacho kimefunguliwa mwezi Januari, 2025 na kimeanza kutoa huduma kwa wananchi wa Paje na maeneo jirani.

e) Baraza la Mji Kati limekamilisha ujenzi wa Bustani ya Jamii katika eneo la Jumbi ambayo imeshazinduliwa rasmi na ina uwezo wa kuchukuwa watu 200 kwa wakati mmoja. Aidha, ujenzi wa Bustani ya Jamii Hanyengwa Mchana unaendelea na umefikia asilimia 70.

f) Baraza la Mji Kaskazini “B” limekamilisha ujenzi wa Soko la Kitope lenye uwezo wa kuchukua wajasiriamali 150. Aidha, Baraza limekamilisha maandalizi ya ujenzi wa Soko la Mahonda ambapo mkataba wake umeshawasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

g) Baraza la Mji Wete limefanikiwa kuanza kujenga Soko la Mzambarauni ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 50. Aidha, Baraza limefanikiwa kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa kiwanja cha kufurahishia watoto kitakachojengwa eneo la Weni na kuendeleza taratibu na lengo la ujenzi wa Soko la Kojani.

h) Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imefanikiwa kujenga vituo vinne vya kusubiria daladala katika maeneo ya Tondooni, Mjini Wingwi, Tumbe na Micheweni. Aidha, Halmashauri imekamilisha maandalizi ya mradi wa ujenzi wa kiwanja cha kufurahishia watoto Tumbe na maandalizi ya ujenzi wa Soko la Micheweni.

i) Baraza la Mji Mkoani, limefanikiwa kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa Soko la Kengeja ambaye ni Kampuni ya Ujenzi ya Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ).

j) Baraza la Manispaa ya Mjini limeanza kujenga Soko la Kwa Haji Tumbo na limeshirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) kujenga Soko la Mombasa.

k) Baraza la Manispaa ya Magharibi “B” limekamilisha maandalizi ya ujenzi wa maegesho katika eneo la Mombasa Sokoni, pamoja na maandalizi ya ujenzi wa Soko katika Jimbo la Dimani.

**6) Utekelezaji wa miradi ya Wadi**

73. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya Waheshimiwa Madiwani katika ngazi ya Wadi kupitia fedha za makusanyo

ya mapato ya ndani. Miradi iliyotekelezwa imejumuisha ujenzi wa madarasa, uchimbaji wa visima, uwekaji wa taa za mitaani, ujenzi wa vivuko na miundombinu mbalimbali.

## G. MAFANIKIO YA WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII

### 1) Kuunganisha mfumo wa usajili wa matukio ya kijamii na mifumo mengine ya Taasisi.

74. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilipanga kuunganisha mfumo wa usajili wa matukio ya Kijamii na mifumo ya taasisi 15 ambapo hadi kufikia Machi 2025, jumla ya taasisi 15 zilizopangwa ziliweza kuunganishwa sawa na asilimia 100 ya utekelezaji. Uunganishaji huu umeongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa kurahisisha upatikanaji wa taarifa za wananchi pindi zinapohitajika, kupunguza ucheleweshaji na kuhakikisha usahihi wa taarifa katika taasisi husika. Miongoni mwa Taasisi zilizounganishwa mifumo yake na mfumo wa usajili wa matukio ya kijamii ni Kamisheni ya Ardhi (Land Transfer System), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Benki ya CRDB, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

### 2) Kufanya uhakiki wa vyeti vya kuzaliwa mtandaoni (Online Certification)

75. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii imeanzisha huduma ya uhakiki wa vyeti vya kuzaliwa mtandaoni ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi. Kwa kipindi cha miezi tisa jumla ya maombi 4,462 yamepokelewa na kufanyiwa kazi. Huduma hii imepunguza msongamano ofisini, imeimarisha usalama wa taarifa na kupunguza uwezekano wa udanganyifu, hivyo kuongeza ufanisi wa mfumo wa usajili wa matukio ya kijamii Zanzibar.

**3) Kuweka mifumo ya kiusalama ya usajili wa matukio ya kijamii**

76. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2025, Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii imefanikiwa kuboresha kituo cha uidhinishaji wa taarifa za matukio ya kijamii (Approval Center), hatua ambayo imeongeza ufanisi na umakini wa maafisa katika kukamilisha usajili wa matukio ya kijamii. Uboreshaji huu umeimarisha mifumo ya kiusalama, kupunguza makosa ya usajili, na kuhakikisha kuwa taarifa zote zinahakikiwa kwa usahihi kabla ya kuthibitishwa, hivyo kuongeza uaminifu wa mfumo wa usajili wa matukio ya kijamii.

**4) Kuhuisha kumbukumbu za zamani kwa kuziingiza katika mfumo wa sasa wa usajili wa matukio ya kijamii**

77. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii, kwa kipindi cha miezi tisa ilikadiria kuhuisha kumbukumbu za zamani 150,000 na hadi kufikia Machi 2025 jumla ya kumbukumbu 140,127 sawa na asilimia 93 zimehuishwa kwa kuingizwa katika mfumo wa sasa wa kidijitali wa usajili wa matukio ya kijamii.

**5) Kutungwa kwa kanuni za ulinzi wa taarifa za matukio ya kijamii**

78. M**heshimiwa Spika,** Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii iliazimia kutunga kanuni za ulinzi wa taarifa za matukio ya kijamii kwa mwaka wa fedha 2024/25, na hadi kufikia Machi, 2025 kanuni hizo zimeweza kutungwa na kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua zaidi. Kuwepo kwa kanuni hizo kutasaidia kuzuia matumizi mabaya ya taarifa na kuongeza uaminifu katika mfumo wa usajili wa matukio ya kijamii Zanzibar.

**6) Kukamilisha Mpango Mkakati wa Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii**

79. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii imeweza kukamilisha kuandaa mpango mkakati wa Ofisi yake, hatua ambayo ni muhimu katika kuhakikisha utendaji kazi unakua wa ufanisi zaidi. Mpango kazi huu unatoa dira, malengo, na mikakati ya muda mfupi na mrefu ili kuboresha utoaji wa huduma za usajili wa matukio ya kijamii.

**7) Kutoa elimu ya usajili wa matukio ya kijamii**

80. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii ilipanga kutoa vipindi 12 kupitia televisheni na redio hadi kufikia Machi 2025, jumla ya vipindi 9 vimetolewa sawa na asilimia 75 ya utekelezaji. Jumla ya skuli za Sekondari 12 na vyuo vikuu viwili vimepatiwa elimu ya usajili wa matukio ya kijamii. Skuli zilizopatiwa elimu ya usajili wa matukio ya kijamii ni Skuli ya Kiembe Samaki, Skuli ya Mahonda, Skuli ya Kiponda, Skuli ya Hamamni, Skuli ya Mkwajuni, Skuli ya Hasnuu Makame, Skuli ya Jang'ombe, Skuli ya Mombasa, Skuli ya Neo leera, Skuli ya Feza, Skuli ya Lumumba na Skuli ya Sekondari ya Dkt. Ali Mohammed Shein. Kwa upande wa vyuo ni Chuo kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kampasi ya Pemba.

## H. MWELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

81. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ itaendelea kutekeleza Programu Kuu 30 kupitia Mafungu 12 ambayo ni D01 hadi D12 yatakayotekelezwa na Ofisi za Makao Makuu, Idara Maalum za SMZ, Ofisi za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii.

82. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kipaumbele cha Ofisi hii kupitia Kamati za Usalama za Mikoa na Wilaya zinazoongozwa na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya pamoja na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na vyombo vyengine vya ulinzi na usalama ni kuhakikisha amani na utulivu inakuwepo wakati wote wa maandalizi na ufanyikaji wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, kwa lengo la kuhakikisha nchi yetu inaendelea kubakia kuwa ya amani na utulivu ili kuendeleza harakati za maendeleo.

## I. MALENGO YATAKAYOTEKELEZWA NA MAKAO MAKUU (D01)

83. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Afisi kupitia fungu la bajeti la Makao Makuu (D01) imepanga kutekeleza malengo yafuatayo;

a) Kuendeleza utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama Zanzibar ili kuhakikisha amani inaendelea kushamiri wakati wote.

b) Serikali imepanga kuanza rasmi ujenzi wa Mradi wa Kituo cha Mabasi ya Kisasa na Maegesho katika eneo la Bwawa la Mwanakwerekwe.

c) Kuendeleza ujenzi wa Chuo cha Mafunzo Hanyegwa Mchana.

d) Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Masheha ambapo zaidi ya Ofisi 100 zitajengwa Unguja na Pemba.

e) Kuratibu ujenzi wa Mradi wa ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

f) Kuendelea kuratibu Mradi wa Pemba Kijani unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya kwa Miji ya Chake Chake, Mkoani, Wete na Micheweni.

g) Kuimarisha usajili na uratibu wa Jumuiya zisizo za Kiserikali (NGOs) Zanzibar.

h) Kutekeleza mradi wa kuimarisha usafi katika Mji ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya usafi, ununuzi wa vifaa vya usafi na kupendezesha mji.

i) Kusimamia utekelezaji wa mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ngazi ya jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Benki ya Dunia.

j) Kukamilisha mchakato wa upatikanaji wa Sheria mpya ya Utumishi wa Idara Maalum za SMZ.

k) Kuimarisha utendaji kazi wa viwanda vya Idara Maalum za SMZ.

l) Kumaliza kuyapima maeneo yote ya Kambi za Idara Maalum za SMZ.

m) Kuyaangalia upya maslahi ya Waheshimiwa Madiwani na Waheshimiwa Masheha.

n) Kuanza maandalizi ya ujenzi wa masoko ya kisasa Kibandamaiti Unguja na soko la Chake Chake Pemba. Masoko haya yatafanana na masoko ya kisasa ya Jumbi na Mwanakwerekwe.

o) Kuanza maandalizi ya mradi wa uimarishaji wa Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar.

## J. MALENGO YATAKAYOTEKELEZWA NA IDARA MAALUM ZA SMZ (D02-D06)

84. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Jeshi la Kujenga Uchumi (D02), Chuo cha Mafunzo (D03), Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (D04), Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (D05) na Kikosi cha Valantia Zanzibar (D06) malengo yatakayotekelezwa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni kama ifuatavyo;-

a. Jeshi la Kujenga Uchumi limepanga kuanza ujenzi wa jengo la Kisasa la Makao Makuu ya JKU Saateni, kuendeleza ujenzi wa mahanga ya Maafisa na Wapiganaji katika eneo la JKU Ng'ambwa Pemba na kuanza kujenga Dahalia ya Skuli ya Sekondari na Skuli ya Ufundi JKU Mtoni. Aidha, Jeshi la Kujenga Uchumi litatekeleza mradi wa ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Wakala wa Ulinzi JKU Mtoni pamoja na kuiboresha Wakala wa Ulinzi JKU kwa kuipatia vitendea kazi vya kisasa.

b. Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimepanga kuimarisha nguvu za ulinzi wa doria na uokozi baharini, kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo ni ujenzi wa kituo cha uzamiaji na uokozi Kizimkazi, ununuzi wa vifaa vya uzamiaji na uokozi, kuanza maandalizi ya ujenzi wa Makao Makuu ya KMKM Kibweni, kutekeleza ujenzi wa hanga la Wapiganaji KMKM Bwefum pamoja na kuzifanyia ukarabati kambi zake Unguja na Pemba.

c. Chuo cha Mafunzo kimepanga kuimarisha huduma za urekebishaji tabia kwa wanafunzi, kuimarisha shughuli za kilimo kwa kuweka mifumo ya umwagiliaji na kuendelea na Mradi wa Mahanga ya Askari Hanyengwa Mchana na Langoni. Aidha, Chuo cha Mafunzo kimepanga kununua magari ya kubebea wanafunzi na mahabusu kwa kuwapeleka na kuwarejesha katika vyombo vya sheria.

d. Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimepanga kufanya ukaguzi wa usalama wa moto katika majengo, kuimarisha huduma za uokozi na uzimaji moto katika maeneo ya utalii na uwekezaji pamoja na viwanja vya ndege, kuendeleza ujenzi wa vituo vya zimamoto na uokozi, ujenzi wa mahanga ya Wapiganaji, kuanza maandalizi ya ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Zimamoto Kilimani na kusimamia upatikanaji wa vitendea kazi ikiwemo magari ya zimamoto.

e. Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ) kimepanga kukamilisha ujenzi wa mahanga na Ofisi, ujenzi wa hospitali za KVZ Mtoni na Ndugukitu na kuanza ujenzi wa kiwanja cha mpira cha kisasa cha KVZ Mtoni. Vile vile, Kikosi kimepanga kuimarisha doria na operesheni za ulinzi na usalama.

f. Kuimarisha ulinzi na usalama wakati wote wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 kuanzia maandalizi yake mpaka kumalizika kwake.

g. Kutoa mafunzo ya Kijeshi kwa Maafisa na Wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ

h. Kuimarisha shughuli za utamaduni na michezo ikiwemo michezo ya Majeshi BAMATA.

i. Kuimarisha huduma za afya katika kambi za Idara Maalum za SMZ.

j. Kubuni na kuimarisha miradi ya uzalishaji mali.

k. Kuendelea kuyapima na kuyapatia hati miliki maeneo ya kambi za Idara Maalum za SMZ.

l. Kuanza maandalizi ya mradi wa ujenzi wa uzio kwa kambi zote za Idara Maalum za SMZ.

m. Kuendeleza hatua za maandalizi ya ujenzi wa barabara zinazoingia katika kambi za Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

n. Kuendelea kuchukua hatua za kuimarisha utendaji kazi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi katika Viwanja vya ndege.

## K. MALENGO YATAKAYOTEKELEZWA NA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA 2025/2026

85. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Afisi za Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Afisi za Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya zimepanga kutekeleza malengo yafuatayo;-

a. Kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu kupitia Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa, Wilaya na Shehia katika kipindi chote cha maandalizi na ufanyikaji wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

b. Kuendelea kusimamia amani na utulivu ili kuhakikisha wananchi wanafanya shughuli zao za kimaendeleo, kiuchumi na kijamii.

c. Kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali ndani ya Mikoa.

d. Kutoa huduma za utawala na uendeshaji katika ngazi ya Mkoa, Wilaya na Shehia

e. Kusimamia utendaji kazi na uwajibikaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa

f. Kuendelea kushirikiana na sekta mbali mbali za Serikali na binafsi kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Mikoa.

g. Kufuatilia utekelezaji wa ahadi na maagizo ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kufuatilia ziara wanazozifanya kwenye Mikoa na Wilaya.

86. **Mheshimiwa Spika,** katika usimamizi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa malengo yafuatayo yamepangwa kutekelezwa;

a) Kuimarisha usafi wa mazingira kwa kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu na vifaa vya usafi pamoja na kufanya shughuli za usafi kwa utaratibu wa kutumia kampuni binafsi.

b) Baraza la Manispaa Mjini limepanga kuendeleza na kukamilisha mradi wa ujenzi wa Soko la Kwahaji tumbo awamu ya kwanza.

c) Baraza la Manispaa Magharibi "A" limepanga kuanza mradi wa ujenzi wa Stendi ya Daladala Mambosasa, kuanza maandalizi ya mradi wa ujenzi wa kiwanja cha kufurahishia watoto Chuini na kuanza ujenzi wa kituo cha mafuta katika eneo la Mbuzini Unguja.

d) Baraza la Manispaa Magharibi "B" limepanga kuanza ujenzi wa maegesho mkabala na Soko la Mombasa na kuanza ujenzi wa Soko katika Jimbo la Dimani.

e) Baraza la Mji Kati limepanga kujenga kituo cha kusarifu taka Chwaka, litaendeleza ujenzi wa vituo vya daladala na limepanga kukamilisha ujenzi wa bustani ya jamii Hanyengwa Mchana.

f) Halmashauri ya Wilaya ya Kusini imepanga kuanza mradi wa kujenga Stendi ya daladala Makunduchi.

g) Manispaa ya Kaskazini "A" imepanga kukamilisha ujenzi wa Soko la Chaani, kufanya ukarabati mkubwa wa Soko la Kinyasini na kuanza maandalizi ya ujenzi wa kiwanja cha kufurahishia watoto Nungwi.

h) Baraza la Mji Kaskazini "B" limepanga kuanza ujenzi wa Soko la Mahonda na kuendeleza kukamilisha taratibu za ujenzi wa Soko la Bumbwini.

i) Manispaa ya Chake Chake imepanga kukamilisha ujenzi wa maegesho Tibirinzi, kufanya ujenzi wa vituo vya daladala, kuliimarisha jaa la Vitongoji pamoja na kujenga ukuta (uzio) wa Bustani ya Mwanamashungi.

j) Baraza la Mji Mkoani limepanga kuanza na kukamilisha ujenzi wa Soko la Kengeja pamoja na kujenga vituo vitano vya kusubiria daladala katika barabara ya Ole-Kengeja.

k) Baraza la Mji Wete limepanga kukamilisha mradi wa ujenzi wa Soko la Mzambarauni na kuanza ujenzi wa Soko la Kojani. Aidha, Baraza la Mji Wete limepanga kuanza ujenzi wa Kiwanja cha kufurahishia watoto Weni na kuanza maandalizi ya ujenzi wa bustani ya Jamhuri Wete.

l) Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imepanga kuanza ujenzi wa Soko la Micheweni ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa wananchi wa Micheweni.

## L. MALENGO YATAKAYOTEKELEZWA NA WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII KWA MWAKA 2025/2026

87. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Wakala wa Usaji wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (D12) kwa mwaka wa fedha 2025/2026 umepanga kutekeleza malengo yafuatayo;

a) Kuanza ujenzi wa Kituo cha urejeshaji wa huduma za matukio ya Kijamii baada ya majanga (Disaster Recovery Center).

b) Kuanza ujenzi wa Ofisi ya Usajili wa Matukio ya Kijamii ya Wilaya ya Kaskazini "B" Mahonda.

c) Kuingiza kumbukumbu za zamani za usajili katika Mfumo wa Usajili wa Matukio ya Kijamii kwa njia ya kielektroniki (CRVS).

d) Kufanya mapitio ya mkataba wa huduma kwa wateja.

e) Kuendelea kutoa elimu ya usajili wa matukio ya kijamii.

f) Kuendelea kusajili matukio ya kijamii Zanzibar kwa wakati na ufanisi.

## M. MAOMBI YA KUIDHINISHIWA MAPATO NA MATUMIZI KWA KILA FUNGU (DO1-D12) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

88. **Mheshimiwa Spika,** ili kuweza kutekeleza malengo yaliyokusudiwa, naliomba Baraza lako kuidhinisha mapato na matumizi ya Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kila fungu la bajeti kuanzia D01 hadi D12 kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama ifuatavyo;-

89. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 100,616,970,000 kwa fungu D01 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Katibu Mkuu wa Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Kati ya fedha hizo, Shilingi 2,272,300,000 ni mishahara, Shilingi 5,920,800,000 ni matumizi mengineyo, Shilingi 301,900,000 ni ruzuku ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ na Shilingi 92,121,970,000 ni kazi za maendeleo ambapo kati ya hizo Shilingi 81,750,000,000 ni fedha za SMZ na Shilingi 10,371,970,000 ni fedha za Wahisani. Aidha, fungu hili linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi 1,800,000,000 yatakayokusanywa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

90. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 71,852,300,000 kwa fungu D02 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Kamanda Mkuu wa Jeshi la Kujenga Uchumi. Kati ya fedha hizo Shilingi 46,715,900,000 ni mishahara, Shilingi 9,864,000,000 ni matumizi mengineyo, Shilingi 738,300,000 ni ruzuku ya Wakala wa Ulinzi JKU na Shilingi 14,534,100,000 ni kazi za maendeleo. Aidha, fungu hili linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi 3,079,418,000 yatakayokusanywa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambapo Shilingi 2,700,000,000 zitakusanywa na Wakala wa Ulinzi JKU na Shilingi 379,418,000 zitakusanywa na Jeshi la Kujenga Uchumi.

91. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 41,992,700,000 kwa fungu D03 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Kamishna wa Chuo Cha Mafunzo. Kati ya hizo Shilingi 31,788,900,000 ni mishahara, Shilingi 6,625,800,000 ni matumizi mengineyo na Shilingi 3,578,000,000 ni kazi za maendeleo. Aidha, Fungu hili linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi 297,089,000 yatayokusanywa kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

92. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 69,655,300,000 kwa fungu D04 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Kamanda Mkuu wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo.Kati ya fedha hizo Shilingi 55,200,000,000 ni mishahara, Shilingi 9,455,300,000 ni matumizi mengineyo na Shilingi 5,000,000,000 ni kazi za maendeleo. Aidha, Fungu hili linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi 290,763,000 yatayokusanywa kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

93. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 54,538,957,000 kwa fungu D05 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Kamishna wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi. Kati ya fedha hizo Shillingi 24,951,100,000 ni mishahara, Shillingi 3,827,800,000 ni matumizi mengineyo na Shilingi 25,760,057,000 ni kazi za maendeleo ambapo kati ya hizo Shilingi 5,550,000,000 ni fedha za SMZ na Shilingi 20,210,057,000 ni fedha za Wahisani (mkopo). Vile vile, Fungu hili linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi 458,138,000 yatayokusanywa kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

94. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 44,864,900,000 kwa fungu D06 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Kamanda Mkuu wa Kikosi Cha Valantia Zanzibar. Kati ya fedha hizo Shillingi 35,027,500,000 ni mishahara, Shillingi 4,313,400,000 ni matumizi mengineyo na Shilingi 5,524,000,000 ni kazi za maendeleo.

95. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 13,500,600,000 kwa fungu D07 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Mjini Magharibi. Kati ya fedha hizo Shilingi 2,603,200,000 ni mishahara, Shilingi 1,946,200,000 ni matumizi mengineyo na Shilingi 8,951,200,000 ni ruzuku ya Serikali za Mitaa. Kati ya fedha hizo za ruzuku Shilingi 1,316,300,000 zitatumika kwa Baraza la Jiji, Shilingi 4,555,700,000 zitatumika kwa Baraza la Manispaa ya Mjini, Shilingi 1,495,100,000 zitatumika kwa Baraza la Manispaa Magharibi "A" na Shilingi 1,584,100,000 zitatumika kwa Baraza la Manispaa Magharibi "B".

96. **Mheshimiwa Spika,** Fungu D07 linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi 80,504,000 yatakayokusanywa kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, Fungu D07 linaomba kuidhinishiwa mapato ya ndani Shilingi 3,880,000,000 yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Manispaa ya Mjini, mapato ya ndani ya Shilingi 2,530,000,000 yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Manispaa Magharibi 'A' na mapato ya ndani ya Shilingi 2,901,674,000 yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Manispaa ya Magharibi 'B'.

97. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 4,710,577,000 kwa fungu D08 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kusini Unguja. Kati ya fedha hizo Shilingi 1,893,500,000 ni mishahara, Shilingi 1,010,477,000 ni matumizi mengineyo na Shilingi 1,806,600,000 ni ruzuku ya Serikali za Mitaa. Kati ya fedha hizo za ruzuku Shilingi 907,600,000 zitatumika kwa Baraza la Mji Kati na Shilingi 899,000,000 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini.

98. **Mheshimiwa Spika,** Fungu D08 linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi 58,561,000 yatakayokusanywa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, Fungu

D08 linaomba kuidhinishiwa mapato ya ndani ya Shilingi 1,955,000,000 yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Mji Kati na mapato ya ndani ya Shilingi 1,243,740,000 yatakayokusanywa na kutumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kusini.

99. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 5,614,500,000 kwa fungu D09 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kaskazini Unguja. Kati ya fedha hizo Shilingi 2,098,700,000 ni mishahara, Shilingi 998,200,000 ni matumizi mengineyo na Shilingi 2,517,600,000 ni ruzuku ya Serikali zake za Mitaa. Kati ya fedha hizo za ruzuku Shilingi 1,254,900,000 zitatumika kwa Baraza la Manispaa Kaskazini "A" na Shilingi 1,262,700,000 zitatumika kwa Baraza la Mji Kaskazini 'B'.

